



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

KULAANI KITENDO CHA UKIUKWAJI WA MAADILI YA KITAALUMA  
KWA MUUGUZI AMOS MATHIAS (LESENI No. 32266)

Dodoma, Agosti 18, 2023.

Baraza la Uuguzi na Ukunga ni Mamlaka ya Kisheria iliyanzishwa kwa ajili ya usimamizi wa taaluma na wanataaluma ya Uuguzi na Ukunga nchini. Lengo la kuanzishwa chombo hiki ni kuhakikisha jamii inapata huduma zilizo bora na salama kutoka kwa wauguzi na wakunga. Baraza linafanya kazi chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga (*The Nursing and Midwifery Act of 2010*).

Baraza limepata taarifa ya Muuguzi AMOS MATHIAS aliyejikuwa amesajiliwa kwa leseni Na. 32266 ambayo ilikuwa imekwisha muda wake toka Mwaka 2016, kuwa amehukumiwa kifungo cha miaka 15 jela. Taarifa ya chombo cha habari iliyochapishwa Agosti 16, 2023 na Gazeti la Habari leo Mtandaoni imesema kuwa Mahakama Kuu ya Kanda Tabora imemtia hatiani **Bw. Amos Mathias** kwa kosa la kuua. Bwana Amosi alidanganya watu kuwa yeye ni Daktari, hivyo kumfanyia upasuaji wa tumbo na sehemu za siri za Mzee mwenye umri wa miaka 78 ambaye alikuwa na tatizo la Ugonjwa wa Ngirimaji.

Aidha imebainika kuwa Bw. Amos alikuwa akitoa huduma nyingine kama kung'oa meno, kufanya tohara na upasuaji wa watu majumbani, huku akiwa hana taaluma hiyo kinyume na mawanda yake yaani (*scope of practice*). Huduma hizi alikuwa akizitoa katika mazingira hararishi, vitendo ambavyo ni kinyume na taratibu, miongozo kanuni na sheria za kitabibu.

Baraza la Uuguzi na Ukunga **linalaani** vitendo alivyofanya muuguzi huyu kwakuwa vinadhalilisha taaluma ya uuguzi na kusababisha madhara mengi hadi kusababisha kifo cha mtu.

*Ammosi*


**Kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010, kifungu cha 25(2)(c) Muuguzi Amos Mathias amepoteza sifa ya kuendela kuwa muuguzi, na kuruhusiwa kutoa huduma kwa wananchi. Hivyo shauri lake litapelekwa katika kikao cha Baraza kwa ajili ya kuliondoa jina lake katika Orodha ya wauguzi na kufuta leseni yake.**

Kwa niaba ya Baraza la Uuguzi na Ukunga natoa pole kwa familia waliyopoteza mpendwa wao na wale wote walioathirika na vitendo vya muuguzi huyu.

Natoa rai kwa wauguzi na wakunga wote nchini, kuhakikisha wanaendelea kutoa huduma kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria ikiwa pamoja na kuzingatia maadili ya kitaaluma. Wataalam waache kabisa vitendo viovu vya kutoa huduma kinyume na ujuzi na mawanda yao.

Tunawahakikishia wananchi kuwa Baraza litaendelea kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa Wauguzi na Wakunga ambao wanakiuka maadili ya taaluma zao, matendo kama haya yanaiaibisha taaluma ya Wauguzi ambao ni kiungo katika upatikanaji wa huduma bora za matibabu.

Imetolewa na:



Agnes Mtawa

**MSAJILI WA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA  
TANZANIA**